



TAHADHARI YA KUZUIA KUENEA KWA COVID-19 KWA WADAU, NAHODHA WA MASHUA/BOTI, BAHARIA NA ABIRIA

Virusi vya Corona (COVID-19) ni familia ya virusi vinavyosababisha magonjwa kama homa ya kawaida hadi magonjwa hatari zaidi. COVID-19 ni aina mpya ya virusi ambavyo havijawaitambuliwa hapo awali kwa wanadamu. Virusi hivi vinaenea kutoka kwa mtu aliyeambukizwa kupitia:

- Matone ya kupumua yanayotokana wakati unapokohoa au kupiga chafya
- Kukaribiana na kugusa au kushikana mikono, kisha kugusa mdomo wako, pua au macho
- Kugusa sehemu zilizo na virusi, kisha kugusa mdomo wako, pua au macho

Dalili za COVID-19 zinaweza kuchukua hadi siku 14 kudhihirika baada ya kuambukizwa na virusi, hii ni pamoja na dalili kama homa, kukohoa, maumivu ya kichwa, maumivu ya mwili na ugumu wa kupumua.

Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) limetathmini Ugonjwa wa Coronavirus 2019 (COVID19) kuwa janga. Serikali inachukua hatua ya kupunguza maambukizi katika jamii na kuzuia mlipuko inapowezekana.

Ili kupunguza athari za COVID-19, kila mtu ana jukumu la kutekeleza. Inachukua zaidi ya serikali na hatua kutoka kwa sekta ya afya kulinda afya na usalama wa wananchi na raia wa inchi za kigeni wanaoishi humu nchini.

Kila mmoja wetu anaweza kusaidia nchi yetu kuwa tayari kwa kuelewa jinsi ya kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa coronavirus. Kutokana na maagizo ya Serikali, Kenya Maritime Authority inawahimiza nahodha, wamiliki, waangalizi na wafanyikazi wa boti na abiria kuchukua hatua zifuatazo za tahadhari ili kupunguza hatari ya kuambukizwa COVID-19.

1. KUTOKARIBIANA

Kufanya uzoefu wa kutokaribiana na wenzio ili kuzuia au kupunguza maambukizi ya COVID19, unapojisikia vibaya unaombwa kukaa nyumbani.

Virusi vya COVID-19 vinaenea haraka kwenye sehemu zilizo na umati wa watu. Kuongezeka kwa magonjwa yanayoambukiza kunaweza kusababisha shida zaidi kwenye mfumo wa utunzaji wa afya wakati wa milipuko. Kwa hivyo tunahimiza kutokaribiana kwenye mashua na kutoabiria chombo kilicho na umati wa watu.

Wamiliki na waendeshaji wa mashua na boti wameelekezwa kupunguza kiwango cha abiria kwenye mashua kwa asilimia sitini (60%) kwa maagizo ya Serikali ili kusikuwe na kukaribiana kwenye mashua na boti.

2. KUTUMIA NJIA MBADALA KUSALIMIANA

Kwa kuwa virusi vya kupumua, kama ile inayosababisha COVID-19 uenea kupitia mawasiliano ya karibu, badilisha jinsi unavyosalimiana. Badala ya kusalimiana na mikono, kubusu au kumkumbatia mwenzio, tunashauriwa kupungiana hewani ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa COVID-19.

3. USAFI

Fanya uzoefu wa kunawa mikono na sabuni mara kwa mara nakudumisha adabu ya kupiga chafya. Safisha vitu vinavyoguswa mara kwa mara kwenye boti, kama vile usukani, reli za mikono na viti.

Nahodha, mabaharia na abiria wanashauriwa;

- a) Kuzingatia usafi bora wa kibinafsi;
- b) Kuzoea kunawa mikono kwa sabuni mara kwa mara;
- c) Kusafisha mara kwa mara boya la kuokoa maisha (life jacket) kutumia kiambukua (disinfectant)
- d) Kuvaa barakoa (mask) ikiwa una dalili za kukohoa
- e) Kufunika mdomo na karatasi ya tishu wakati wa kukohoa au kupiga chafya, na kutupa karatasi ya tishu iliyotumika kwenye pipa la takataka mara moja;
- f) Kutafuta matibabu haraka ikiwa unajisikia vibaya
- g) Kupunguza kukaribiana kwenye boti/mashua.

4. MIKUTANO YA HADHARA

Kwa Maagizo ya Serikali, mikutano ya hadhara imesimamishwa. Wahudumu wa mashua na boti wanahimizwa kuweka hatua mwafaka yakutimiza maagizo ipasavyo

5. VIFAA VYA KINGA YA KIBINAFSI

Vifaa vya kinga ya kibinafsi (PPE), kama vile barakoa (masks) ya aina ya upasuaji na glavu za aina ya matibabu, inapaswa kutumiwa kwa msingi wa mfiduo wa hatari na kwa kufuata mwongozo wa afya ya umma na mwongozo wa afya na usalama wa kazini kwa COVID-19.

Usafi wa mikono ndiyo njia bora ya kuzuia kuambukizwa, ikumbukwe kwamba utumiaji usiofaa wa glavu unaweza kutoa hisia za uwongo za usalama na kuongeza hatari ya kuambukizwa.

6. WASAFIRI WAGONJWA

Dalili za kawaida za COVID-19 ni Homa ya mapua, joto mingi mwilini, Kikohozi na ugumu wa kupumua.

Wamiliki na wafanyikazi wa mashua na boti ambao watagundua abiria yeyote ambaye anaonyesha dalili za COVID-19 wanapaswa:

- a) Kutoa ripoti kwa timu za dharura za Wizara ya Afya kupitia nambari zifuatazo: 0800721316, 0729471414, 0732353535, 719 kwa msaada sahihi wa matibabu na mwongozo
- b) Kupatia barakoa (mask) ya upasuaji abiria ambaye hajihisi vizuri.
- c) Kuvaa barakoa (mask) ya upasuaji wakati unahudhuria abiria ambaye hajihisi vizuri.
- d) Kubadilisha barakoa (masks) ikiwa imechafuka.
- e) Ikiwa barakoa (mask) ya upasuaji haipatikani, abiria anapaswa kufunika mdomo na pua na karatasi ya tishu wakati wa kukohoa.
- f) Barakoa zote na karatasi tishu, zinazotumiwa na abiria ambaye anaonyesha dalili kama za COVID-19 inapaswa kuwekwa kwenye mifuko ya plastiki isiyoweza kuvuja.

7. KUTUNZA AFYA YAKO

Mtu yeyote ambaye atakuwa na dalili kama za COVID-19 anapaswa kutoa ripoti kwa timu za dharura za Wizara ya Afya kupitia nambari zifuatazo: 0800721316, 0729471414, 0732353535 kwa msaada sahihi wa matibabu na mwongozo mara moja.



Maj. (Rtd) George N. Okong'o
DIRECTOR GENERAL